



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA
MAJIMBO MAWILI NA UDIWANI KATIKA KATA NNE -
TANZANIA BARA

Tume ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 aliitaarifu Tume uwepo wazi wa Jimbo la Kinondoni katika Jiji la Dar Es Salaam na Jimbo la Siha katika Mkoa wa Kilimanjaro. Majimbo haya yamekuwa wazi kufuatia Ndugu Maulid Mtulia Mbunge wa Jimbo la Kinondoni Kujiuzulu uanachama wa Chama cha CUF na Dr. Godwin Mollel Mbunge wa Jimbo la Siha kujiuzulu Uanachama wa CHADEMA.

Hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 67 (1) (b) na 71 (1) (f) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani ya mwaka 1977 inaeleza kuwa iwapo Mbunge atajivua uanachama atapoteza sifa ya kuwa Mbunge.

Vile vile, Tume imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi

za Madiwani katika Kata nne (4) za Tanzania Bara. Kata hizo ni:-
 Kata ya Isamilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana Mkoa wa Mwanza, Kata ya Manzase katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma, Kata ya Madanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani Mkoa wa Tanga na Kata ya Kimagai katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapa Mkoa wa Dodoma.

Kwa kuzingatia matakwa ya vifungu vya 37 (1) (b) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, pamoja na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kuwa majimbo mawili na Kata nne zipo wazi.

Orodha ya Majimbo na Kata zilizowazi ni hizi zifuatazo:-

Majimbo ya Uchaguzi yaliyowazi:

NA.	MKOA	HALMASHAURI	JIMBO
1.	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	Siha
2.	Dar es Salaam	Halmashauri ya Wilaya Wilaya ya Kinondoni	Kinondoni

Kata zilizowazi:

N A.	MKOA	HALMASHAURI	KATA
1.	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana	Isamilo
2.	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	Manzase
3.	Tanga	Halmashauri ya Wilaya ya Pangani	Madanga
4	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	Kimagai

Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya vifungu vya 37(1)(b) (5) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, pamoja na vifungu vya 13(3) na 41(3) vya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume inatoa taarifa ya Ratiba ya uchaguzi mdogo katika majimbo mawili na Kata nne, kama ifuatavyo

- 1. Kutoa fomu za uteuzi kwa majimbo hayo mawili na kata nne itakuwa kati ya tarehe 14 hadi 20 Januari 2018,**
- 2. Uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 20 Januari 2018,**

- 3. Kampeni za Uchaguzi huu mdogo zitaanza tarehe 21 Januari na kumalizika tarehe 16 Februari 2018, na**
- 4. Siku ya Uchaguzi itakuwa tarehe 17 Februari 2018**

Tunawakumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na maelekezo yote wakati wa kipindi cha Uchaguzi mdogo wa Majimbo mawili na Kata Nne.

Imetolewa leo tarehe 03 Januari, 2018.

Mhe. Jaji Mkuu (Mst. Zanzibar) Hamid Mahmoud Hamid

MAKAMU MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI